HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

SIMU(MKUU WA SHULE) SHULE YA SEKONDARI ULIWA
NA. 0622936536/0623753599 S.L.P 719
Kumb. Na. ULSS/F.I/VOL I/ 2020 NJOMBE
TAREHE 18/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI _____

. **YAH . MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ULIWA WILAYA YA NJOMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021**

1.0 UTANGULIZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika Shule hii mwaka 2021 . Shule ya sekondari ya Uliwa ipo umbali wa km 50 kusini mwa Halmashauri ya mji Njombe kijiji cha Uliwa, Kata ya Iwungilo, Tarafa ya Igominyi na unachepukia Uwemba na kuacha barabara kuu iendayo Ludewa.

Usafiri wa basi kutoka mjini Njombe unapatikana kila siku katika kituo cha mabasi cha Njombe mjini na nauli ni Tsh. 5000/=.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 10/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/01/2021.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. SARE ZA SHULE

(a)WAVULANA

1.Mashati mawili meupe tetroni mikono mirefu.
2.Suruali moja ya rangi ya damu ya mzee.
3.Suruali moja (1) ya kijani
4.Suruali moja (1) rangi nyeusi kwa ajili ya kazi za mikono
5.Fulana (T-shirt)moja (1) rangi ya bluu
6.Sweta rangi ya bluu yenye shingo ya V
7.Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2)
8.Soksi rangi nyeusi jozi mbili (2)
9.Raba za michezo jozi moja (1)
10.Bukta moja ya michezo rangi ya bluu
11.Track suti nyeusi
NB: Suruali ya heshima yenye malinda,mifuko 3 na isiyobana. Tofauti na hapo utashona Upya. kitambaa aina ya ESTEEM NAMBA MOJA

(b)WASICHANA

1.Vigauni viwili (2), rangi ya damu ya mzee kimoja na kijani kimoja vya kuvalia suruali vyenye mikono mifupi,havina kola ila vina malinda. kitambaa aina ya ESTEEM NAMBA MOJA .(Angalia mchoro)
2.Suruali tatu (2) moja rangi ya damu ya mzee,ya pili rangi ya kijani.
3.Sweta rangi ya bluu yenye shingo ya V
4.Viatu nyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi jizi mbili (2)
5.Soksi ndefu (stockings)rangi nyeupe jozi mbili (2)
6.Raba za michezo jozi moja (1)

7.Tight ya michezo
8.Bukta moja rangi ya bluu
9.T-shert ya bluu
10.Track suti nyeusi moja (1)
11. Gauni moja rangi ya zambarau urefu iwe inavuka magoti,mshono wa solo (kitambaa aina ya ESTEEM NAMBA MOJA)
12. Mashati mawili meupe tetroni mikono mirefu.

Nguo za ndani na mahitaji maalim ya mtoto wa kike viwe vya kutosha.
NB: Suruali ziwe ndefu za heshima zenye malinda na mifuko mitatu. Ikishonwa tofauti utatakiwa kushona upya.

2.2. VIFAA VYA DARASANI

1.Madaftari 10 Counter book Q3
2.Mkebe na vifaa vyake (Mathematical set)
3.Kalamu za wino na penseli za kutosha
4.Kamsi moja (1) ya kiingereza kwa kiingereza)
5.Bunda moja ya karatasi photocopy A4 kwa ajili ya majaribio, mazoezi,mitihani n.k.
6. Graph paper kijitabu kimoja

2.3. MAHITAJI YA HOSTELI

Shule hii ni ya kutwa, hata hivyo wanafunzi wote wanakaa hapa shuleni katika mabweni (Hosteli),kwa sababu eneo hili halina nyumba za kupanga pia ni makubaliano ya wazazi kwamba wanafunzi wote wakae bwenini. Hivyo unatakiwa kuleta mahitaji yafuatayo,

* MALAZI

1.Godoro moja futi 2 ½ aina ya DODOMA
2.Mashuka mawili (2) pinki
3.Blanketi moja
4. ***Wavulana*** *waje na Ndoo moja (1) lita 10,jembe jipya lenye mpini,soft broom1 na chelewa 1 kwaajili ya usafi binafsi na shughuli nyingine.*
Wasichana *waje na Ndoo moja (1) lita 10,jembe jipya lenye mpini,mopper 1 na chelewa 1 kwaajili ya usafi binafsi na shughuli nyingine*.

CHAKULA

Wanafunzi wote hupata huduma ya chakula shuleni. Kwa kuwa mwanafunzi hana muda wa kujipikia chakula chake mwenyewe.Vyakula vyote huchangwa na wazazi/ walezi, hivyo unatakiwa kuleta michango ya chakula kama ifuatavyo.

1.Mahindi debe 12 au kilo 240 kwa mwaka au debe 6 au kilo 120 kwa mhula
2.Maharage debe 3 au kilo 60 kwa mwaka au debe 1½ au kilo 30 kwa mhula
3.Mchele kilo 20 kwa mwaka au kilo 10 kwa mhula
4.Fedha ya kuendeshea hosteli wapishi Tshs 141,000/= kwa mwaka au shilingi 73,000/= kwa mhula, kwa ajili ya kulipa wapishi, kuni, umeme na viungo.
5.Vyombo vya chakula kama sahani,bakuli,kikombe na kijiko

NB: Shule haina huduma yoyote ya chakula maalumu kwa wanafunzi wenye matatizo Kiafya.

Malipo ya fedha ya hosteli na huduma ya kwanza yafanyike kwa njia ya Benki,kwenye akaunti ya Shule NMB kama ifuatavyo: Namba ya akaunti **60610003669,** Jina la akaunti Uliwa secondary.

Zingatia maelekezo ya fomu ya kuwekea fedha pale benki, kwa mfano. Andika kwa usahihi Namba ya akaunti, jina la akaunti kiasi cha fedha kwa ajili ya (Hosteli na huduma ya kwanza) ya (Taja jina la mwanafunzi), jina la mwekaji na sahihi.
Nakala halisi ya fomu ya kuwekea na siyo photocopy ilete shuleni. Shule haitapokea fedha taslimu.

MALIPO YAFANYIKE KAMA IFUATAVYO
Mhula wa kwanza **jumla Tsh. 73000**/= Mhula wa pili **Tsh.68000/=**

2.4.HUDUMA YA KWANZA: Kila mwanafunzi atapata huduma ya kwanza shuleni ila matibabu mengine atajitegemea.

2.5. NAULI: Nauli ya kuja Shuleni na kurudi nyumbani atajitegemea.

NB:Kumbuka shule ya Uliwa Sekondari ni ya kutwa yaani (day), Lakini shule inatoa huduma ya Hosteli kutokana na umbali kutoka vijiji na shule hivyo mzazi/mlezi unasisitizwa kulipia mahitaji ya Hosteli mara tu mtoto anaporipoti shuleni. Mtoto hatapokelewa Hosteli endapo mzazi/ mlezi hujachangia mahindi, mchele, maharage na fedh.

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama Ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo Yote inayotolewa na wizara ya elimu,sayansi na teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo nakala yake Utapewa.

a)Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b)Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c)Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d)Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f)Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;
g)Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i)Kutunza mali za umma
j) Utoro

3.1.**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a) Wizi wa aina yoyote.
b)Uasherati,uhusiano wa jinsi moja,kuoa au kuolewa
c)Ubakaji
d)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi

kubeli na kadhalika.

e)Kupigana au kupiga
f)kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g)Kudharau Bendera ya Taifa
h)Kuwa mjamzito /kupata mimba au kusababisha mimba
i)Kuoa au kuolewa
j)Kutoa mimba
k)Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l)Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Nikosa kubwa kwa mwanafunzi kutembelea katika majumba au maeneo ya sterehe mfano,vilabu vya pombe,baa na nyumba za kulala wageni
n)Kuwa na simu ya mkononi.
o) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

4.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

a)Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara unaporipoti Shuleni.
b)Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi.
c)Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na Shule.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

_____

MKUU WA SHULE.